kenyaeducators@gmail.com

# KCPE WARM UP

## MAZOEZI YA MADA ZOTE (DARASA LA NANE)

For marking schemes call Mr machuki 0795491185

### ZOEZI A: UMOJA NA WINGI

*Andika sentensi zifuatazo katika wingi.*

1) Wembe umevunjika.
2) Mtume hufanya kazi ga Mungu.
3) Mchuzi rojorojo hupendeza.
4) Uyoga ukipikwa hulika.
5) Mjusi ameanguka kutoka mtini.
6) Ungwele umenyolewa na kingozi.
7) Mkunga anamsaidia mama.
8) Mkunga amemvua mkunga mkubwa.
9) Kikulacho ki nguoni mwako.
10) Utamu wa asali ni mwema.

### ZOEZI B VIVUMISHI

Bainisha vivumishi vilivgopigiwa mstari Vjvumishi vua sifa

1) Magari mapya uote gamenunuliwa.
2) Kikulacho ki Wapi?
3) Ubao wetu umepakwa rangi nyeusi
4) Unaelekea wapi?
5) Mtoto wa jirani ameumia sana.
6) Majina yote uataandikwa upya.

For more e-learning resources 0795491185

7) Mabao hayo ni mengi mno.
8) Kuku wale ndio wenge vifaranga.
9) Viatu vivi hivi ndivyo vyangu.
10) Chakula hiki hiki ni kitamu.
11) Magaidi wote ni sharti waangamizwe.
12) Mwenye macho haambiwi tazama.
13) Shilingi mia tano zitalipwa na kila mmoja.
14) Je, umemwaga maji yote?
15) Mavazi **yale** ni sharti yafanane na haua.

ZOEZI C: VIELEZI

Chagua vielezi vya jinsi

*Kila wakati, shuleni, katika twa! Shaghalabaghala, shuleni, kortini,*

*usiku, mara tatu, zaidi, tena, kijinga, duKani, njiani, usiku mkuu,*

*tamu, kesho kutwa, taratibu. Wakati huu, Saa nne*

ZOEZI D. WINGI NA UMOJA

Andika sentensi zifuatazo katika wingi au katika umoja

1) Wewe umesimama wima.
2) Mtoto atalia mwenyewe.
3) Sisi tumealikwa karamuni.
4) Nyinyi hamjasoma
5) Nuinyi m watoto wachanga, ZOEZI E: UKANUSHAJI

Kanusha sentensi zifuatazo

1) Wewe hujasoma kwa bidii.
2) Wao hawataadhibiwa na mwalimu.
3) Mimi sitaandaliwa chakula kingine.

4) Wewe unampenda rafiki yako.
5) Wajinga ndio waliwao

ZOEZI F: MATUMIZI YA KI

Bainisha matumii ya KI katika sentensi zifuatazo

a) Ukichezu utafeli mtihani.
b) Akiondoka nitaenda kulala.
c) Mbona unakula kitoto?
d) Kitoto hiki ni kijinga.
e) Utakula ukicheza?
f) Watakapofika nitakuwa nikiandika.
g) Anacheza akirukaruka
h) Paka akiondoka panya hutawala
i) Kikulacho ki nguoni mwako.
j) Anapenda kuvalia Kiafrika,

ZOEZI G TASHBIHI

Kamilisha tashbihi zifuatazo

1) Pendana kama
2) Chukiana kama
3) Tamu kama
4) Kigeugeu kama
5) Laini kama
6) Chungu kama
7) Mbio kama
8) Thamini kama
9) Adimika kama
10) Gonga kama 11) Chafu kama
12) Embamba kama

13)Nene kama

14) Nona kama

15)Mkali kama

16)Mbio kama

17)Tamu kama

18)Nyeupe kama

19)Msiri kama

20)Safi kama

21)Metameta kama

22)Maridadi kama

23)Fura kama

24)Nzito kama 25) Nuka kama

26)Pendeza kama

27)Chukiwa kama

28)Mpole kama

29)Thamini kama

30)Randaranda kama

31)Wauawaga kama

32)Lia kama

33)Angaza kama

34)Takatifu kama

35)Tetea kama

36)Aminika kama

ZOEZI H: UUNDAJI WA MANENO-VITENZI

Unda majina Kutokana na vitenzi vifuatavyo

a) Tema………………….

b) Osha……………………….

c) Kula …………………

d) Pika……………………

e) Kata…………………..

f) Apa…………………

g) Jua …………………

h) Ogopa ………………

i) Ita…………………

j) Lia………………..

ZOEZI I: KAULI

Andiko vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendesha

1) Kata
2) Ona
3) Kimbia
4) Fanua
5) Dadisi
6) Enda
7) Shiba
8) Lala
9) Pika
10) Imba

ZOEZI J

Kamilisha jedwali lifuatalo

| Wastani (kawaida) | Ukubwa | Udogo |
| --- | --- | --- |

| | | |
|---|---|---|
| a) Mguu<br>b) Kalamu<br>c) Siafu<br>d) Kioo<br>e) Kinywa<br>f) Ndume<br>g) Mkono<br>h) Ngumba<br>i) Meza<br>j) Chumba | | |

## ZOEZI K: USEMI WA TAARIFA

**Badilisha sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa**

a) "Mimi simpendi Kurecho kwa sababu ya wizi wake," Kamene alisema.
b) "Njoo tusaidiane," Mwangi alimuita Okech.
c) "Sisi sote tuna mahitaji getu," Wanachama walimwambia mkurugenzi.
d) "Maisha ya sasa yanahitaji mpango mwema," baba alitushauri.
e) "Tutaondoka kesho asubuhi," alisema.

## ZOEZI L: USEMI HALISI

**Badilisha sentensi zifuatazo katika usemi halisi**

a) Karanja alisema kwamba angemwona angemwita.
b) Nyanya alisema kuwa wangeenda sokoni siku hiyo.
c) Mwenyekiti alitangaza kuwa mkutano ungeanza saa nne na nusu.
d) Mwalimu alisema wangeandika insha siku hiyo.
e) Daktari alimwambia kuwa alikuwa na vipele.

Taja vikembe vya Wanyama wafuatao

| Mnyama | kikembe |
|---|---|
| 1) N'gombe | |
| 2) Nguruwe | |
| 3) ndege | |
| 4) punda | |
| 5) Simba | |
| 6) paka | |
| 7) Sungura | |
| 8) Mbwa | |
| 9) Nyuki | |
| 10) Bata | |

| | |
|---|---|
| 11)papa | |
| 12)Nyoka | |
| 13)Kipepeo | |
| 14)Tai | |
| 15)Nyani | |
| 16)Ngamia | |
| 17)Kuku | |
| 18)Farasi | |
| 19)Chui | |
| 20)Ndovu | |
| 21)Mamba | |
| 22)Fisi | |
| 23)Farasi na punda | |
| 24)Mdudu | |
| 25)Nzi | |
| 26)Nyangumi | |
| 27)Nge | |
| 28)Kondoo | |
| 29)Mbu | |
| 30)Nzige | |
| 31)Mbweha | |
| 32)Mbuzi | |
| 33)Chungu | |

<u>Kamilisha vifungu vifuatavyo vya mkusanyiko wa vitu vikiwa pamoja</u>

1) Hadhara ya …………………..
2) Hukumu ya……………
3) Halaiki ya…………………….
4) Sisisi ya ………………….

5) Hombo la ………………….
6) Mtungo wa ……………………..
7) Numbi ya ………………..
8) Thurea ya
9) Mlolongo wa
10) Kipeto cha
11) Maktaba ya
12) Kicha cha
13) Kipeto cha
14) Chane ya
15) Funda la
16) Tone la
17) Kidimbwi cha
18) Tama la
19) Karne ya
20) Doti ya
21) Jopo la
22) Tone la
23) Fala la
24) Biwi la
25) Korija la
26) Mzengwe wa
27) Koja la
28) Bumba la
29) Kidani cha
30) Gora ya
31) Msitu wa
32) Sharafa la
33) Minofu ya 34) Wingu la
35) Cheche za

36)Jora ya

37)Mkungu wa

38)Shungi la

39)Tita la

40)Kikundi cha

41)Kikoa cha

42)Tano ya

43)Kambi la

44)Shumbi la

45)Safu ya

46)Kambi ya

47)Halmashauri ya

48)Tanuu ya

49)Kipini cha d

50)Nakidi ya

51)Jozi ya

52)Robota la

53)Kikataa cha

54)Mannunyu ya

55)Kamati ya

56)Kichala cha

57)Kifurushi cha

58)Kitata cha

<u>ZOEZI LA MASHAIRI</u>

1) Shairi la mshororo mmoja huitwa?
2) Ushairi wonyc beti nyingi na hauna vina vya kati?
3) Shairi lenye mizani kumi na sita kila mshororo na mishororo minne huitwa?
4) Shairi ambalo halikufuata kanuni za utunzi ndilo?
5) Kifungu cha maneno cha shairi huitwaje?

6) Mshororo wa tatu huitwaje?
7) Gwiji wa kuimba mashairi anaitwaje?
8) Jina la kubandikwa katika ushairi linaitwaje?
9) Taja vipande vitatu vya mshororo mmoja.
10) Keketo au mlingano wa sauti unaitwaje?
11) Mstari unaojirudiarudia huelezea nini shairini?

JIBU MASWALI HAYA YANAYOHUSIANA NA NYAKATI ZA SIKU - WAKATI MAALUM

i. Mapambazuko / macheo / mawio Kunakucha ili kuanze siku mpya huitwa ……………….
ii. Majogoo kwenye saa tisa ni…………………………..
iii. Saa kumi na saa kumi na moja alfajiri ni…………………………..
iv. Baada ya alfajiri / mafungulia ngombe / Saa mbili hadi saa nne asubuhi ni…………………….
v. Katikati ya mchana, wakati wa jua la utosi / wakati wa mtikati ni……………….
vi. Kipindi cha kuanzia saa moja hadi saa tatu usiku ni……………………..

JIBU MASWALI HAYA YANAYOHUSIANA NA MISIMU

1) ……………ni Kipindi cha mwaka chenye jua kali na joto jingi. Huwapo baina ya vuli na masika.
2) ……………. Kipindi cha joto na mvua nyingi.
3) ……………….ni Kipindi cha baridi kali.
4) ………………… ni Majira ya mvua ndogondogo kati ya Julai na oktoba.
5) …………………….ni Msimu wa upepo unaovuma kutoka Kaskazini Mashariki na wenye joto kali hasa katika uwanda wa pwani.
6) ………………ni Kipindi cha mvua fupi ziletwazo na upepo 7) …………….ni pepo za Magharibi.
8) ……………ni pepo za Kusini.
9) ………………ni pepo za Mashariki.
10) ………………ni pepo za Kaskazini.

KAMILISHA JEDWALI KWA SAUTI NA MILIO YA VIUMBE NA VITU VIFUATAVYO

| Kiumbe/mnyama/ kitu/hali Fulani | Mlio/matokeo ya hali fulani |
|---|---|

| | |
|---|---|
| 1) Ng'ombe.<br>2) Mbwa<br>3) Simba.<br>4) Chui,<br>5) Nyoka<br>6) Tembo<br>7) Upepo<br>8) Moto<br>9) Kondoo<br>10) Farasi<br>11) Nyuni<br>12) Miti ………………wakati wa upepo.<br>13) Kengele<br>14) Saa<br>15) Kithembe<br>16) Mlevi<br>17) Fisi<br>18) Tembe<br>19) Mtu …………………maudhini.<br>20) Kitata<br>21) Mchawi<br>22) Punda<br>23) Nyasi kavu zinazoteketea<br>24) Chungu jikoni<br>25) Mkanyago wa majani makavu<br>26) Kuongea lugha isiyoeleweka<br>Kukorokocha | |

| | |
|---|---|
| 27)Sauti ya kusitasita<br>28)Mlio wa ngoma<br>29)Sauti ya bomu<br>30)Sauti ya bunduki, bastola/ risasi<br>31)Kutoa sauti usingizini unapoota<br>32)Kutoa pumzi kwa nguvu<br>33)Kusema maneno ya matusi<br>34)Kupigapiga mbawa<br>35)Ng'ombe hucheua na panya hu….<br>36)Nyoka hutambaa na jongoo hu……….<br>37)Sauti ya mtu aliye usingizini<br>38)Mlio wa hatari wa meli vitani jeshini<br>39)Mlio mkali wa hofu kana kwamba unateswa<br>40)Nyuki<br>41)Mbu | |

JIBU MASWALI HAYA YANAYOHUSIANA NA SIKU MAALUMU

1) Siku iliyotangulia jana huitwa………………………… 2) Siku kabla ya leo ni…………………

3) Siku tuliyonayo; siku hii ni………………………..
4) Siku inafuata ni………………………………….
5) Siku baada ya kesho huitwa……………………..
6) Siku inayofuata keshokutwa ni………………………….
7) Siku inayofuatia mtondo; siku ya nne baada ya leo ni………………………….

ZOEZI LA RANGI

1) Rangi ya majani yasiyo makavu yaitwaje?

2) Usiku wenye giza tororo huashiria rangi ipi?
3) Rangi ya limau lililoiva huitwaje?
4) Kaniki nyingi huwa ni za rangi gani?
5) Kijani hafifu ni rangi ipi hiyo?
6) Rangi ya samsi ni rangi gani?
7) Andika visawe vitatu vya hudhurungi.
8) Ngeu huwa ya rangi gani?
9) Andika rangi ya dhahabu.
10) Umbijani ni rangi ya?

## TAJA MAPAMBO MANNE YANAYOVALIWA KATIKA SEHEMU ZIFUATAZO ZA MWILI

1) Masikioni
2) Kichwani
3) Puani
4) Kifuani
5) Shingoni
6) Madini
7) Mikononi
8) Miguuni
9) Usoni
10) Kiunoni

## FAFANUA MAGONJWA YAFUATAYO

1) Tauni
2) Malale
3) Tetewanga
4) Shurua
5) Ndui
6) Ukoma
7) Kifafa
8) Kipindupindu / waba

9) Kaswende / Seneneko

10)Kifua kikuu
11)Pepopunda

12)Homa ya matumbo

13)Malaria

14)Kichocho

15)Kuhara

16)Kupooza

17)Sotoka

18)Homa iletwayo na chawa

19)Saratani

20)Kimeta

21)Matende

22)Utapiamlo

23)Kifaduro

24)Manjano

25)Kupooza 26) Nyongoa

27)Safira

28)Machumbwi

29)Choa

30)Lalab 31) Jibu

32) Pumu

33) pele

<u>ZOEZI (UKOO)</u>

1) Wazazi wa mke na mume wanaitanaje?
2) Wanaume waliooa nyumba moja huitanaje?
3) Nyumba ya wake wengi inaitwaje?
4) Nitamwitaje m ke wa mjomba?
5) Kinyume cha halati ni?

6) Mtoto wa kaka yako utamwitaje?
7) Dada humwitaje mke wa kaka yake?
8) Mtoto wa kitukuu huitwaje?
9) Usiyeweza kuoana nayo 10) Kaka na dada huitanaje.

MASWALI YANAYOHUSIANA NA MAENEO YA UTAWALA

1) ………………… Huongozwa na naibu wa chifu.
2) ………………….. Huongozwa na chifu, '
3) ……………..Huongozwa na mudiri / Kaunti ndogo.
4) …………………. Huongozwa na Gavana.
5) …………………. Huongozwa na rais.

MASWALI YANAYOHUSIANA NA UHUSIANO WA WATU NA NCHI

a) Anayeipenda nchi yake na yu tayari kuipigania ni…………………..
b) Aichukiaye nchi yake hata kutoa siri zake kwa adui ni…………………………
c) Anayekimbia nchi yake kutokana na matatizo kama vita ni……………………
d) Anayetoroka nchi yake labda kwa sababu ya kisiasa ………………………
e) Anayetembea nchi yake kwa madhumuni ya kujionea kustarehe ni……………………
f) Anayepeleleza mambo ya nchi nyingine kisirisiri huitwa …………………………..
g) Anayewakilisha nchi yake katika nchi nyingine ni………………………..
h) Anayeihamia nchi nyingine na kufanya makao ya huko nii……………….
i) Anayeitawala nchi nyingine isiyo yake ni…………………………….
j) Aliyezaliwa katika nchi fulani ni……………………………….
k) Aliyezaliwa mahali fulani na akaendelea kukaa huko ni………………………
l) Ambaye amejitolea kufanya kazi ya ulinzi ni…………………………….
m) Mwenyeji wa nchi fulani ni………………………………………
n) Anayetumiwa na kiongozi mwingine kwa manufaa ya kiongozi huyo ni……………………………
o) Anayefuata mfano wa utawala wa mabavu ni…………………………….
p) Asiyependa mabadiliko ni…………………………….
q) Anayetangulia kuanzisha jambo ni……………………………….

## MASWALI YANAYOHUSIANA NA MAHAKAMA

### Jaza pengo

1) ……………..hutoa hukumu.
2) ……………………ni Aliyeleta malalamiko mahakamani.
3) ……………………ni Aliyedaiwa / Kufikiriwa ndiye mwenye kosa.
4) ……………………ni Anayetoa ushahidi, aliyeona / kusikia tukio husika.
5) ……………………ni Anayemtetea mshtaki / mshtakiwa. Kiongozi wa korti — Anayeomwongoza na kuelekeza mkondo wa kesi.
6) ……………………ni Anayeandika matukio kortini.
7) ……………………ni Anayedhaniwa kuwa amehusika katika uhalifu fulani.
8) ……………………ni Aliyehukumiwa kifungo gerezani / Jelani.
9) ……………………ni Hakimu anayeshughulikia mahakama fulani.
10)……………………ni Mshauri mkuu wa serikali kuhusiana na mambo ya sheria.
11)……………………ni Wakili wa kuendesha mashtaka mahakamani.
12)……………………ni Mlalamishi anayepigania haki yake kutoka kwa mdaiwa.
13)……………………ni mtu anayetakiwa alipe aonyeshe kitu cha mwingine 14) ……………………ni Mshukiwa aliyefikiriwa amefanya kosa.
15)……………………ni Kesi iliyo na uzito mkubwa kamakesi ya mauji.
16)……………………ni Kesi kutokana na kupanga njama ya kupindua serikali.
17)……………………ni Kesi dhidi ya mtu mmoja na mwengine.
18)……………………ni Kukataa kukubiliana na kesi.
19)……………………ni Kukata kesi Kutoa hukumu-kuamua kesi.
20)……………………ni Kuomba kesi isikilizwe upya.
21)……………………ni Malipo yanayotolewa na mshtakiwa ili
22)……………………ni Fedha iniyotozwa kama adhabu kwa mwenye hatia.
23)……………………ni Sehemu katika karti anamokaa mshtakiwa , mshtaki / shahidi.
24)……………………ni Uamuzi katika kesi.
25)……………………ni Seli ya kuwafungia washukiwa katika kituo cha polisi.

26)……………………ni Sehemu maalum katika jela wanamowekwa mahabusu ambao kesi hazijakamilika / husuni / gereza.

27)……………………ni Wanapofungwa mahabusu wanapotumikia kifungo chao.

28)……………………ni Vikuku Vyuma vya duara vya kufungia wahalifu hususan mikononi.

MASWALI YANAYOHUSIANA NA MSAMIATI WA JIKONI

Kamilisha jedwali

| MAELEZO AULA | NENO |
|---|---|
| 1) Mahali pa kuanikia kuni au vitu; kichaga 2) Kifuu cha nazi cha kukorogea mchuzi.<br>3) Chombo cha kukaangia maakuli.<br>4) Bakuli la kuoshea mikono.<br>5) Kifaa cha bapa cha kusongea ugali<br>6) Sinja ya mbao ya kupakulia chakula.<br>7) Chombo cha kauri au mabati, hutiliwa chai.<br>8) Kamba ya kuninginizia nyungu.<br>9) Bomba la kutolea moshi.<br>10) Kifaa cha kukunia nazi.<br>11) Kifaa cha kuchotea maji<br>12) Mkeka wa mviringo na huanikia chakula.<br>13) Kifaa chenye tundu cha kupepetea chakula.<br>14) Chombo cha kutwangia nafaka.<br>15) Mti wa kutwangia kwenye kihu.<br>16) Mtungi wa udongo au kauri; | Uchaga/utaa |

## MASWALI YA ZIADA YA JIKONI

1) Mimi hutumika kuokea mikate.
2) Chombo cha kuchujia tui huitwaje?
3) Tendo la kutoa chakula motoni kiivapo huitwa?
4) Jer unga wa ugali huitwaje kwa jina jingine?
5) Unga wa makaa yaliyochomeka, una majina. Taja mawili.
6) Tendo la kuweka sufurai jikoni ili mlo uanze kuiva 7) Toa maana ya kanza.

8) ……………..ni mseto wa mahindi na mandondo. 9)

Kifaa cha kuchujia nazi kina majina matatu, yatajeø

10) Mchele mweupe uliopikwa huitwa?

11)Mimi ni sinia ya mbao ya kupakulia madhishi. Naitwa?

12)Bakuli la kuoshea mikono huitwaje?

13)Mimi ni maji makali ya kutia maakulini. Naitwa?

14)Pilipili ndogo inayowasha mno inaitwa pilipili tamu au hoho?

Mimi hutumika kusukumia chapatti.

## ELEZA MATENDO YAFUATAYO JIKONI

1) Kukoka moto
2) Kupuliza moto
3) Kuzima moto
4) Kuteleka / kuinjika
5) Kuepua / kuinjua -
6) Kutokosa
7) Kutokota
8) Pepeta
9) Oka
10) Banika
11) Kanza

## MASWALI YANAYOHUSIANA NA VYOMBO KATIKA KARAKANA

### Kamilisha jedwali lifuatalo

kenyaeducators@gmail.com

| Matumizi | Chombo | Anayetumia |
|---|---|---|
| 1) Uzi wa kupimia urefu<br>2) Mfuko wa kutumia ku uliza moto<br>3) Kifaa cha kugongomelea | | |
| 4) Kutobolea mashimo kwenye mbao<br>5) Chombo cha kutobolea mbao<br>6) Chombo cha kusawazisha mbao<br>7) Karatasi ngumu ya kusawazisha mbao<br>8) Randa ya kuviringa mbao<br>9) Nyundo kubwa ya mbao<br>10) Chombo cha kukereza / kukata mbao<br>11) Kutolea/ kuingiza misumari kukazia skrubu<br>12) Kushikilia vitu imara vinapofanyiwa kazi<br>13) Kifaa cha kufanyia michoro<br>14) Kutobolea matundu<br>15) Kupimia na kufanyia mistari<br>16) Kunolea vyombo<br>17) Msumeno mkubwa unaoshikwa na watu wawili<br>18) Sindano ya kushonea kiatu<br>19) Nyundo ndogo ya mbao ya kutengenezea kiatu<br>20) Chombo cha kupimia urefu<br>21) Kupimia usawa au unyookaji wa kitu<br>22) Kifaa cha kutumia kidoleni wakati wa kushona<br>23) Udongo wa kujengea nyumba<br>24) Jiwe la kutilia makali shoka, panga, makasi na kisu<br>25) Kuchongea mbao<br>26) Kushikia vitu vinavyoundwa<br>27) Chuma anachotumia mhunzi kuwekea chuma anachofua. | | |

For more e-learning resources 0795491185

## MASWALI YANAYOHUSIANA NA MAUMBILE YA NCHI

1) ……………..ni Bonde lenye maji yanayotiririka wakati wote.
2) …………………..ni Sehemu yenye maji mengi iliyozungukwa na nchi kavu.
3) …………………..in Eneo kubwa la maji ya chumvi linalozungukwa na nchi kavu.
4) …………………….ni Sehemu ya pwani ambayo maji hujaa na hupwaa.
5) …………………ni Sehemu ya mto unapojigawanya vipande viwili au zaidi unapoingia baharini.
6) ………………..ni Mahali penye tope au telezi.
7) ……………………ni Mahali maji yanapobubujika.
8) ……………………….ni Mteremko mkali wa kwenye kingo za mto.
9) ……………….ni Eneo la nchi kavu lililozungukwa na maji.
10) ……………ni Eneo kubwa lililo na miti mingi.
11) ……………….ni Sehemu inayoota nyasi na miti midogo. Jangwa Eneo kubwa na kame ambalo kwa kawaida huwa na mchanga lisiloota nyasi wala miti.
12) ……………………ni Nchi isiyokuwa na miinuko wala mabonde.
13) ……………ni Bonde Sehennu ya ardhi iliyo katikati ya vilima viwili.
14) ……………..ni kilele Sehemu ya juu kabisa ya mlima.
15) …………….ni Mlipuko mkali wa moto unaotokea ndani ya dunia zaha ambayo mara nyingi husababisha milima katika uso wa dunia.
16) …………………ni Sehemu inayopatikana juu ya mlima.
17) ……………….ni Kisima cha jangwani.
18) ……………….ni Eneo la nchi kavu lililozungukwa na maji.
19) ……………………ni Sehemu ya pwani iliyo na mikoko ambapo maji hujaa na kupwa.
20) ………………..ni Sehemu kubwa ya bahari iliyoingia ndani ya pwani.

21)…………………ni Mahali palipochimbuliwa madini.

22)………………..ni Mahali penye miti mifupimifupi iliyoshonana na nyasi.

23)………………..ni Mwamba mkubwa.

## ZOEZI LA HOSPITALINI

1) Chumba cha kungojea umwono tabibu akuhudumie chaitwa ?
2) Andika visawe viwili vya mochari.
3) Dawa udungwayo ili usihisi maumivu wakati unapopasuliwa yaitwa?
4) ………………ni alama ya jeraha iliopona.
5) …………………ni kitengo maalumu hospitalini cha kutibu magonjwa maalumu.
6) ……………..ni chumba cha kufanyia utafiti wa kisayansi hospitalini.
7) Elezea maana ya nyondenyonde.
8) ………….chumba cha kujifungulia wajawazito.
9) …………………..mimi hufanya vitu vidogo visinyoonekana kwa macho viwe vikubwa na
10) umbo na idadi yake.

11)Andika stadi wa kuunga viungo vilivyovunjika.

12)Andika jina la kitanda cha kuchukulia mgonjwa.

13)………………………….hufungiwa jeraha au kidonda.

14)Nikitaka kutoa mtu damu nitatumia kifaa kipi?

15)Toa maana mbili za mkunga.

16)…………………….ni sawa na kufufuka.

17)Kiti cha magurudumu cha kubebea wagonjwa wasioweza kutembea ni…………………

## TOA MAANA NYINGINE YA MANENO YAFUATAYO

1) Baraste
2) Taadhima
3) Msichana
4) Ndoa
5) Stadi.
6) Hamaki
7) Duni

8) Ugali
9) Uliza
10) Rika
11) Aibu
12) Simanzi
13) Baradhuli
14) mpumbavu
15) Hongo
16) chichimiri
17) Afya
18) Kasoro
19) Ukuta
20) Mwizi
21) Mnyama
22) Mvulana -
23) msena
24) Maskini
25) mkata
26) Tajiri
27) Ghani
28) Mwalimu
29) Wasiwasi

## TAJA METHALI NNE NNE ZINAZOOANA NA MAELEZO YAFUATAYO

1) Methali zinazotuhimiza kuwa na bidii:
2) Methali zinazotuhimiza kuwa na uvumilivu
3) Methali zinazotuonya kuhusu tamaa
4) Methali zinazotuon a kutodan an wa na uzuri wa nee
5) Methali zinazotushauri ku ashu hulikia mambo mapema
6) Methali zinazotuliwaza na kutuon esha uwezo wake

7) Methali zinazotuhimiza kutenda mema
8) Methali zinazotuonya kutotumainia mambo kabla litimie
9) Methali zinazotuonya kutotegemea usaidizi wa mbali

MASWALI YANAYOHUSIANA NA MSAMIATI WA MAKAO MAHALI PA KUISHI - HASHUA, KITENDE, MAKAZI

Jibu maswali yafuatayo

1) Makao ya wavulana waliotiwa jando ni……………… 2) Rais huishi kwenye………………….
3) Mfalme huishi kwenye ………………….
4) Mtawala huishi kwenye ……………………
5) Mfungwa hukaa ………………………
6) Makao ya mtu angojeaye kesi ikatwe ………………………
7) Ng'ombe huishi kwenye……………………
8) Samaki huishi …………………..
9) Kasuku huishi kwenye …………………………
10) Kuku huishi kwenye ……………………….
11) Fuko huishi kwenye ……………………
12) Nyuni huishi kwenye …………………………
13) Makao ya kiwavi…………………..
14) Makao ya panzi ……………………
15) Konokono huishi kwenye …………………………
16) Funza huishi ……………………….
17) Mchwa huishi katika …………………. 18) Jana huishi kwenye ……………………
19) Nyuki huishi kwenye…………………..
20) Buibui huishi kwenye…………………
21) Makao ya uchango………………
22) Mahali palipotengwa kuzikia watu…………………..
23) Nyumba ya waislamu …………………..
24) Chumba cha kupokelea wageni……………………

25) Anapotagia kuku………………….

26) Panapoegeshwa magari ……………………

27) Mahali anaposimama mshtakiwa ………………….

28) Mahali pa kupatiwa matibabu madogomadogo…………………. 29) Mahali wanapotahiriwa watoto wa kiume…………………..

30) Wanapojificha wanajeshi kwa ajili ya vita……………….

31) Mahali katika shule wanapolala wanafunzi…………………..

32) Mahali palipohamwa …………….

33) Mahali wanapoogeshwa wanyama ili kuua kupe……………… 34) Anaposimama imamu…………………. 35) Kituo cha kupumzika katika safari ……………… 36) Bweni la wasichana ………………….

37) Mahali wachawi wanapofanya baraza zao za kisiri ………………….

38) Kiunga cha kupanda miti ya…………………..

39) Nyumba ya kuwekea akiba ya chakula au vitu………………….

40) Fungu la nchi kavu lililozungukwa na maji pande zote……………………

<u>ZOEZI LA MALIPO</u>

1) Unapoingia shuleni mara ya kwanza utalipa malipo
2) Pesa serikali ikopeshazo kampuni bila ya riba huitwajo?
3) ………………hulipwa wafanyakazi kila mwisho wa mwezi.
4) ………………………hulipwa kama mali ya posa.
5) …………………. hutolewa kama kitulizo cha hasira. 6) Faida ya kukopesha [pesa yaitwaje?
7) ……………. hawa ni malipo ya kulipia kitu kisinunuliwe na mtu mwingine.
8) ………………. huwa ni malipo ya kumtoa mtu damu. 9) Malipo ya fungu la kumi yaitwaje?
10) ………………………….ni malipo ya kuzunguka mbuyu.
11) Malipo ya pesa za muda uliopita ………………………….
12) Malipo unayompa mtu uliyemwudhi ili kuondoa hasira zake ……………… 13) Malipo kwa ajili ya kumtoa mtu damu ………………………..

14) Mali anayopewa mtu kutokana na mali ya marehemu ……………………

15) Malipo ya kazi ya siku ……………………

16) Fungu la mtaji katika biashara ya ushirikiano ………………………

17) Pesa anazotozyva kulipa mtu aliyekopesha ………………………

18) Kuweka kitu cha thamani kama dhamana ………………

19) Fedha inayotozwa kuwa ni adhabu kwa mwenye hatia ………………………

20) Malipo ya kuonyesha shukrani kwa kutimiza ahadi fulani ………………… 21) Malipo au fungu la nyama apokealo mchungaji…………………….

22) Malipo apokeayo mvulana atokapo jandoni …………………………….

23) Pesa za matumizi ya kila siku ………………….

24) Malipo ya mshukiwa yanayolipwa ili aachiliwe mahakamani ili kesi ifanywe baadaye

25) Malipo kwa ajili ya kupendelewa ………………… <u>TAJA VIUNGANISHI VYA KUONYESHA:</u>

1) Ndani au juu ya katika
2) Wakati
3) Kutojali au ni mamoja
4) Afadhali au bora zaidi
5) Pasipo sababu (pasipo na)
6) Hali ya kinyume
7) Kufuatana na
8) Ubora wa vitu wa kimojawapo
9) Kulinganisha vitu au watu
10) Masikitiko au majuto
11) Hitilafu au kasoro
12) Kuchagua
13) vya sababu
14) kudhania / kutokuwa na
15) viunganishi vya kuongezea

<u>ZOEZI LA SAUTI SI GHUNA AU SAUTI SIGHUNA</u>

1) Chagua kundi la sauti sighuna. *g, ngt h, f, p*

2) Herufi hizi ziko katika kundi lipi la sauti? *M,y,v,r*

3) Ni kundi lipi si la sauti ghuna?

4) A, E, I, O, U huitwaje kwa lugha ya Kiswahili. 5) Chagua sauti ghuna kundini *-V, w, f, p, th, d, g, p*

6) Toa maana ya sighuna.

7) Andika kundi lenye sauti sighuna: *-n, l, d, g, k, chl v, p, v, sh*

8) Neno hili lina sauti ngapi? *Madhara*

9) *dh, ny, ng, gh, sh, th* harufi hizo zina sauti ngapi?

ZOEZI LA SILABI

1) A, E, O, U huitwaje?
2) Andika silabi sahili zozote mbili.
3) Mgi ni la silabi gani?
4) Neno janjaruka lina silabi ngapi?
5) Chagua kundi la silabi ambatano: *mgwi, dwo, ngwe, nyvvt ngo, pwe*
6) Silabi hizi zinaitwaje? *Mbwa, mpwa, ndwo, ngwo* 7) Andika silabi za maneno haya? *We, ze, me, de, ne*, 8) Mdogo ni la silabi ipi?
9) Chagua maneno ya silabi changamano: *mkwe, ng'o, mbwe, nge, mpwa, nywa, nyo ndwi.*
10) Andika kundi la silabi ambatano: *mba, nywi, ngu, pwa, mgwe, mkwe*

KWA MAJIBU PIGA SIMU 0795491185